HOTUBA YA MH. HAWA A. GHASIA (MB.) WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA KATIKA SHEREHE ZA UFUNGUZI WA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA BARANI AFRIKA: DAR ES SALAAM: 16TH JUNE 2009

- ◊ ***Mheshimiwa Ali Shamuhuna, Naibu Waziri Kiongozi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;***
- ◊ ***Mheshimiwa Dalmas O. Anyango, Mwenyekiti wa Mkutano wa Sita wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma Barani Africa;***
- ◊ ***Waheshimiwa Mawaziri Wengine;***
- ◊ ***Mrs Julia Joiner, Kamishna wa Siasa wa Umoja wa Afrika;***
- ◊ ***Waheshimiwa Wabunge;***
- ◊ ***Wawakilishi wa Nchi Mbalimbali;***
- ◊ ***Waheshimiwa Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;***
- ◊ ***Katibu Mkuu Kiongozi;***
- ◊ ***Makatibu Wakuu;***
- ◊ ***Watendaji Mbalimbali wa Serikali;***
- ◊ ***Ndugu Washiriki Wote wa Maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma;***
- ◊ ***Wageni waalikwa;,***
- ◊ ***Mabibi na Mabwana.***

Assalaam Alaykum,

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi kwenye maadhimisho haya ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ambayo kibara yanafanyika Tanzania kuanzia Tarehe 16 hadi 19 Juni 2009; na yale ya kitaifa yanafanyika kuanzia tarehe 16 hadi tarehe 23 Juni 2009. Kuja kwako kwenye sherehe hizi kunatupa heshima. Tunakukaribisha kwa moyo mkunjufu! KARIBU SANA.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Nafurahi kukujulisha kwamba sherehe hizi za kibara (continental) zinahudhuriwa na wajumbe kutoka nchi kumi na mbili (12) za Kiafrika, yaani Kenya, Zimbabwe, Mozambique, Nigeria, Burundi, Rwanda, Algeria, Namibia, Afrika ya Kusini, Gambia, Misri na wenyeji, Tanzania. Aidha, mawaziri watatu ni miongoni mwa wajumbe wanaohudhuria maadhimisho haya. Hawa ni Mh. Dalmas Otieno Anyango, Waziri wa Nchi, Utumishi wa Umma, Jamhuri ya Kenya; Mh. Kajura Hendry Muganwa – Naibu Waziri Mkuu – Uganda, Mh. Prof. E.G. Mukonoweshuru, Waziri wa Utumishi wa Umma, Jamhuri ya Zimbabwe; na Mh. Richard Baloyi, Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Mh. Aman K. Essawi – Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Nchi inayoshughulikia Maendeleo ya Utawala, Misri. Nachukua fursa hii kuwasalimu mawaziri na wajumbe wengine, na KARIBUNI SANA TANZANIA.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Kama nilivyoeleza hapo awali, Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya kibara ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika. Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika kibara husherehekewa na nchi zote za Afrika kila baada ya miaka miwili katika Nchi moja wapo ya Afrika. Mwaka 2007 maadhimisho haya yalifanyika huko Windhoek, Namibia. Pamoja na kusherehekea kwa pamoja, kila Nchi huadhimisha siku hiyo kwa namna inavyoona inafaa ili kutambua umuhimu wa Utumishi wa Umma katika kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wananchi wa Afrika.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Kihistoria Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ilianza mwaka 2001. Mwaka huo ndio mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa umma walikutana huko Windhoek Namibia kuzungumzia masuala yanayohusu utumishi wa umma. Katika mazungumzu hayo mawaziri walikubaliana kwamba nchi za Afrika haziwezi kuendelea kiuchumi bila kuwa na Utumishi wa Umma imara na unaofanyakazi vizuri. Aidha, katika mkutano huo mawaziri waliazimia kwamba shughuli na wajibu wa Utumishi wa Umma lazima utambuliwe na usherehekewe na kila Serikali Barani Afrika.

Kutokana na maamuzi hayo, tarehe 23 Juni ya kila mwaka ilitangazwa kuwa ‘’Siku ya Utumishi wa umma Barani Afrika’’ Kila Nchi ilishauriwa kusherehekea siku hiyo kwa namna ilivyoona inafaa na kwa kutumia Kauli Mbiu iliyokubaliwa na Nchi zote za Afrika.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Maadhimisho haya ya siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika yanayofanyika kibara hapa Tanzania ni sehemu ya maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki moja, yaani tarehe 16-23 Juni 2009. Kama mwenyeji wa maadhimisho haya tumepanga kuwa na shughuli kuu tatu kama ifuatavyo:

(i) Wiki moja ya maonyesho ya bidhaa na huduma ambazo Nchi za Afrika hutoa kwa Wananchi wake;
(ii) Mkutano wa siku mbili wa Mawaziri wa Utumishi wa Umma Barani Afrika; na,
(iii) Kilele cha sherehe hizi za kibara

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Katika shughuli ya kwanza ambayo inahusu maonyesho ya bidhaa na huduma zitolewazo kwa Wananchi wa Afrika, Ukiacha Tanzania, Nchi tatu, yaani Kenya, Zimbabwe na Afrika ya Kusini zinashiriki katika maonyesho haya. Kwa upande wake,Tanzania inawakilishwa na taasisi zipatazo 200 zikiwemo Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala mbali mbali. Napenda kuzishukuru na kuzipongeza taasisi zote za Tanzania na zile za Nchi nyingine kwa kutenga muda wao ili kushiriki katika maonyesho haya.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Mkutano wa siku mbili wa Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma utafanyika Tarehe 17-18 June 2009. Huu utakuwa Mkutano wa 7. Kama nilivyokwisha kusema Mkutano wa Sita ulifanyika mwaka 2008 huko Johannesburg, Afrika ya Kusini. Mikutano mingine ya huko nyuma ni kama ifuatavyo:

(i) Mkutano wa Kwanza – Tangiers, Algeria – 1994;
(ii) Mkutano wa Pili: Rabat, Morocco – 1996;
(iii) Mkutano wa Tatu: Windhoek, Namibia – 2001;
(iv) Mkutano wa Nne: Stellenbosch, Afrika ya kusini – 2003; na,
(v) Mkutano wa Tano: Addis Ababa, Ethiopia – 2005.
(vi) Mkutano wa Sita: Afrika ya Kusini Johannesburg - 2008

Mkutano wa Saba wa Mawaziri wa Utumishi utakaofanyika Dar es salaam utahudhuriwa na mawaziri na maofisa waandamizi kutoka Nchi kumi na mbili (12) za Afrika. Kauli Mbiu ya mkutano huu ni: *''kuimarisha ushirikiano thabiti baina ya serikali na wadau katika utoaji huduma na kuleta maendeleo endelevu Afrika''*

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Kama nilivyosema hapo awali, madhumuni ya shughuli hizi za wiki ya Utumishi wa Umma Barani Afrika ni kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi wa Afrika. Tunaamini kwamba kutokana na kubadilishana mawazo na mrejesho kutoka kwa Wananchi na wadau wengine, maadhimisho haya yatachangia katika kuboresha utoaji wa huduma katika Nchi za Afrika

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

Baada ya maneno hayo machache nakuomba utoe nasaha zako, na kisha utufungulie rasmi sherehe hizi za maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma Barani Afrika

Mheshimiwa Mgeni Rasmi;

KARIBU SANA